

Taarifa kuhusu virusi vya Corona 2019-nCoV

Tangu desemba 2019 katika eneo kubwa la ulimwengu kumeenea coronavirusi mpya. Ugonjwa ambao husababishwa na virusi hivyo vilipata jina la covid-19. Walio wengi huwa wanapata kuumwa maumivu yenye unafuu kidogo ambayo hujitokeza kwa dalili za kushambulia koo la hewa na kawaida huwa dalili hizo hupotea zenyewe, lakini wengine hupatwa na ugonjwa wenye hatari kama uvimbe mchungu katika mapafu/pneumonia. Virusi hiyo humfikia/huambukiza kwa njia ya mawasiliano ya mgusano na mtu aliye mgonjwa au wakati huyo mgonjwa anapokohoa au anapopiga chafya, hiyo inaitwa maambukizi ya matone. Unakuwa na hatari kubwa zaidi kuambukizwa kama ulikuwa katika eneo ambalo limekuwa na kuenea kwa maambukizi au ulikuwa karibu na mtu ambaye alikuwa na maambukizi kutokana na hii coronavirusi mpya.

Mamlaka za nchini Sweden zimetoa wito kwa watu wote wenye dalili za maambukizo katika koo la hewa, hata kama ni ile lainilaini/kidogo, kwamba kuacha kwenda katika mkusanyiko wa watu ambayo itakuwa na hatari ya kusambaza/kueneza maambukizi. Kwa sababu hiyo ni muhimu sana kama unajisikia unakuwa na dalili za kuumwa kama mafua, kukohoa au homa lazima ujitahidi kutokukutana na watu wengine. Usiende kazini, shuleni au chekechea/shule ya awali. Hiyo inahusu hata kama unajisikia kwamba unaumwa kidogo tu. Ni muhimu kwamba usihatarishe kuambukiza wengine.

Hatua za kuzuia

Kama kawaida kwenye hatari za maambukizi ni muhimu sana kuwa muangalifu na usafi. Kwa sababu hiyo ni lazima ufuata njia za kawaida zinazohusu hatua za kuzuia ambazo zipo kwa ajili ya kukinga ili kuto kuwaambukiza wengine, ambazo ni kama:

- Kohoa na piga chafya kwenye kiwiki cha mkono/karibu na kwapani
- Safisha mikono kwa sabuni na maji
- Tumia dawa ya kuuwa wadudu (handsprit)
- Kwepa kukutana na mtu anayeshukiwa kuwa na maambukizi

Kwa taarifa zaidi angalia Muongozo wa Tiba kwenye lugha tafauti:

<https://www.1177.se/other-languages/1177-varldguiden-pa-flera-sprak/>